# MAOMBI

## Ya Kujikuza kiroho

TOLEO LA 3



BY DENIS & DEVIS JULIUS

# <u>MAOMBI MAALUMU YA KUJIKUZA KIROHO</u>

**Toleo ya 3**

**MTU WA NDANI~ Milango ya ufahamu**

## <u>UTANGULIZI:</u>

Mwanadamu ameumbwa katika pande “mama” mbili. Upande wa kwanza ni wa ndani, ambao ndio roho yake ilipo, na wa pili ni ule wa nje ndio mwili wake.
Roho ya mtu inajulikana kama mtu wa ndani. Na mwili wa mtu unajulikana kama mtu wa nje.

Sasa huyu mtu wa ndani huwa anasifa kama tu za mtu wa nje. Isipokuwa tu katika utendaji kazi, kwamba Yule wa ndani hupambanua mambo ya rohoni, Na huyu wa nje hupambanua mambo ya mwilini.

Kama vile mwili wa mtu ulivyo na milango mitano (5) ya fahamu, inayomsaidia mtu kupokea taarifa ya mazingira yanayomzunguka. Yaani:

1. **Macho**
2. **Masikio**
3. **Pua**
4. **Ulimu**
5. **Ngozi**

Vivyo hivyo na roho ya mtu huwa inayo milango hii mitano. Ambayo inamsaidia mtu kupokea taarifa zote za rohoni, zinazoendelea. Hivyo ni muhimu sana, kuhakikisha milango hiyo, ni mizima, na kama sio, basi ni kuomba Bwana akutengeneze, Ili uweze kukamilika, kiroho kama vile ulivyokamilika kimwili.

Tutakuwa tunaangazia na kutoa mwongozo wa kuomba kwa kiungo kimoja hadi kingine kwa mujibu kimaandiko. Kumbuka kuwa maombi haya ni mahususi ya ajili ya ukuaji wako wa kiroho. Ni maombi yasiyopungua SAA SITA (6), Kwa wiki. Si maombi ya dakika 5.

Ni mara nyingi Bwana alituasa “tukeshe tuombe”. Akiwa na maana kuwa tudumu muda mrefu katika sala, kwasababu si kila jambo tutalifikia katika urahisi. Wanaokuwa bora katika michezo, huwa ni wale wanaokaa sana katika mazoezi. Vivyo hivyo na sisi ili tuwe imara rohoni, hatuna budi kudumu sana katika eneo la Maombi, bila kusahau kusoma Neno.

Kila eneo tutaomba kwa muda wa “Saa moja na dakika 15”. = dakika 75

~Mwl Denis & Devis Julius

**MILANGO YA UFAHAMU ~ MTU WA NDANI**

# MACHO. (dk 75)

Yesu alituonyesha jinsi jicho linavyofananishwa na Nuru ya mwilini. Halikadhalika na lile la rohoni vivyo hivyo. Na kwamba likiwa bovu, basi roho yote nayo inakuwa giza. Na madhara ya kuwa kipofu ni kutumbukia shimoni.

**Nuru ya roho:**

*Mathayo 6:22  Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru.23  Lakini jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa na giza. Basi ile nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza; si giza hilo!*

- ✓ Mwombe Bwana akufungue macho yako uione vema nuru yake moyoni mwako. (Ambayo ndio Yesu Kristo). Si wakristo wengi wanaiona nuru hiyo kwa jinsi Bwana anavyotaka waione. Tukifikia kilele cha kuijua yote. Basi rohoni kuenenda kwetu tunabadilishwa na kuwa wengine. Na wala hatutajikwaa kwa lolote kwasababu nuru inamulika sana.

**Tamaa ya macho.** (1Yohana 2:16, 2Petro 2:14)

Macho yana tamaa zake, Unapoona fahari katika uzinzi, uasherati, mali, wizi, ni jicho lako la rohoni ndio linafanya kazi hiyo. Limeacha kupeleka tamaa yake kwenye vitu vya rohoni kama vile upendo, ukarimu, utakatifu. yamekimbilia mambo mengine yasiyopasa.

- ✓ Mwombe Bwana akuondolee tamaa zote za macho. Na fahari za ulimwengu huu. Bali fahari yako iwe kumcha Bwana, jicho lako limwangalie yeye tu.

**Maono:**

*Matendo 2:17  Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto*

Mungu huwa anaweka maono kwenye mioyo ya watu, ambayo yanawapa uwezo wa kutambua na kupanga juu ya nyakati zijazo. Hivyo ukikosa jicho hili la maono la tai linaloona mbali, ni ngumu sana kumshinda adui na hila zake, na pia kufanikiwa mbeleni.

- ✓ Omba Bwana alifungue jicho lako la maono, uweze kuiona yote yanayoendelea rohoni na yanayokuja. Na kuweka mikakato ya ki-Mungu maishani mwako

**Magamba ya macho:**

*Matendo 9:18  Mara vikaanguka machoni pake vitu kama magamba, akapata kuona, akasimama, akabatizwa*

Jambo mojawapo lililomfanya mtume Paulo, kabla ya kuokoka kuwa mpinga-Injili. Ni kwasababu ya magamba ya adui yaliyokuwa yamefunga macho yake asitambue ukweli. Na alipobadilishwa yakaondolewa.

- ✓ Mwombe Bwana ikiwa kuna magamba yoyote yaliyosalia ndani yako, basi ayaondoe. Ili macho yako yaone sawasawa ukweli wote wa injili. Ombea sana eneo hili.

**Jicho la kumtambua Yesu katikati yako/yenu.**

*Luka 24:30  Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa. 31  Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua; kisha akatoweka mbele yao.*

Ni mara nyingi Yesu anasimama katikati yetu lakini hatumtambui kwasababu macho yetu ya rohoni yamefumbwa.

- ✓ Omba Mungu ayafumbue macho yako awapo na wewe karibu katika mazingira yoyote

**Jicho la kuutambua ulinzi wa Mungu juu yako (2Wafalme 6:17)**

Gehazi mtumwa wa Elisha alikuwa na mashaka, kwasababu hakujua kuwa lipo jeshi la malaika wa Bwana limewazunguka. Mpaka Elisha alipomwombea kwa Mungu afunguliwe macho. Na alipofunguliwa aliweza kuliona jeshi lile jinsi lilivyo kubwa sana.

- ✓ Omba Bwana akupe jicho la kuona ulinzi wake, kwako wakati wote, ili uwe na amani ndani yake.

**Uinuliwe macho.**

*Yohana 4:35  Hamsemi ninyi, Bado miezi minne, ndipo yaja mavuno? Tazama, mimi nawaambieni, Inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno*

Macho yakiwa chini hutapata nguvu ya kuona ukubwa au udogo wa kazi uliyowekewa mbele yako. Vilevile hutaona jinsi gani wakati umebaki mchache sana (Soma Luka 21:28).

- ✓ Mwambie Bwana nisaidie macho yangu wakati wote yaelekee mbele na juu, na sio chini. Nipate hamasa ya kuendelea mbele.

**<u>Macho ya kiburi</u>**

*Mithali 6:16 Kuna vitu sita anavyovichukia Bwana; Naam, viko saba vilivyo chukizo kwake. 17 Macho ya kiburi, ulimi wa uongo, Na mikono imwagayo damu isiyo na hatia;*

Kiburi ni ile hali ya kujiinua, kuona kwamba mwingine hawezi kukusaidia. Ni jambo baya ambalo linaweza kukusababishia kutopokea chochote kwa Mungu. Kwasababu anasema huwapinga mwenye kiburi na kuwapa neema wanyenyekevu.

- ✓ Omba Bwana aue jicho la kiburi, uwe mnyenyekevu rohoni kama Kristo alivyokuwa.

<u>**Kijicho:** (Marko 7:22)</u>

Kijicho ni jicho la wivu.Kwamfano pale unapoona mwenzako amepokea upendeleo kama wewe au zaidi ya wewe na hapo hapo unaanza kuona wivu ni mfano wa kijicho. Na hii inamtia mtu unajisi kama Bwana alivyosema.

- ✓ Mwombe Bwana akiue kijicho ndani yako.

Vifungu vingine vya kusimamia, Ni Waefeso 1:18.

**Zingatia:** Bwana alishatuahidi kuwa atatupa "dawa" ya kupaka machoni ili tuweze kuona vema (Ufunuo 3). Hivyo kwa jinsi unavyoomba maombi haya kwa masafa marefu ndivyo unavyompa Bwana nafasi ya kukutia dawa mpaka uone sawasawa. Omba kwa imani ukiwa na kiu kweli ya kufunguliwa macho yako.

## <u>MASIKIO (dk 75).</u>

Kutokusikia vizuri, na kutokusikia kabisa kote kuna madhara. Kwamfano ukikosa kutosikia kabisa huwezi tambua lolote linalosemwa, hata kama ni kwa nguvu kiasi gani. Vilevile kutokusikia vizuri, hupelekea kutokuelewa vinachosemwa.

Bwana anataka masikio yetu ya rohoni, yawe mazima, tusikie vema. Omba

**<u>Masikio yafunguliwe umwelewe Yesu:</u>**

*Mathayo 13:15 Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, Na kwa masikio yao hawasikii vema, Na macho yao wameyafumba; Wasije wakaona kwa macho yao, Wakasikia kwa masikio yao, Wakaelewa kwa mioyo yao, Wakaongoka, nikawaponya*.

- ✓ Omba Bwana Yesu ayatibu masikio yako umwelewe, usiwe kama yale makutano ambayo hayakumwelewa Yesu ijapokuwa yaliishi naye na kumsikia kila siku.Utahiriwe masikio yako.

**<u>Sikio lenye uwezo wa kuelewa:</u>**

*Yohana 12:28  Baba, ulitukuze jina lako. Basi ikaja sauti kutoka mbinguni, Nimelitukuza, nami nitalitukuza tena. 29  Basi mkutano uliosimama karibu wakasikia, walisema ya kwamba kumekuwa ngurumo; wengine walisema, Malaika amesema naye. 30  Yesu akajibu, akasema, Sauti hiyo haikuwako kwa ajili yangu, bali kwa ajili yenu.*

Mungu anaweza kuzungumza na wewe, ukadhani ni mwanadamu, au viongozi, au mfumo, kilele za vitu vya asili n.k. vikaja kama ngurumo kwako,, kumbe ni sauti ya Mungu anataka uelewe jambo Fulani rohoni lakini kwasababu masikio yako hayajaweza kuimbanua sauti ya Mungu, unashindwa kumwelewa.

- ✓ Omba Bwana akupe sikio bora la kuweza kuielewa kwa haraka sauti yake.

**<u>Sikio la kupambanua roho:</u>**

*1Timotheo 4:1  Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani;*

Si kila sauti inatoka kwa Mungu. Hivyo kama sikio lako halina utashi wa Roho kuzipambanua utajikuta unaamini kila fundisho au kila taarifa unayopewa na shetani au mwanadamu.

- ✓ Mwambie Bwana niumbie sikio la upambanuzi wa sauti mbalimbali.

**<u>Utayari wa kusikia</u>**

Wakati mwingine, tunaweza tukawa na masikio ya rohoni yaliyokamilika, lakini hatuna utayari wa kutaka kusikia, tunayafumba masikio yetu wenyewe, au tunaondoka kabisa uwepo mwa Bwana. Na ndio maana Bwana sehemu nyingine alimaliza kwa kusema.. “Mwenye masikio ya kusikia na asikie” (Marko 4:9, Luka 14:35, Ufunuo 13:9)

- ✓ Mwambie Bwana akupe utayari wa kupenda kuyasikia maneno yake.

**<u>Masikio yenye chujio</u>**

*Luka 8:18  “Jiangalieni basi jinsi msikiavyo...”*

Kuwa mwepesi kusikia taarifa zisizojenga, ni rahisi kuiharibu roho yako. Kwamfano taarifa za usengenyaji, miziki ya kidunia, vipindi vya kizinzi  kwenye radio, tv, mtandaoni n.k. huharibu tabia njema.

- ✓ Mwombe Mungu akupe uzito wa kusikia taarifa zisizo na afya kwa roho yako.

## ULIMI (dk 75)

Ulimi ni mlango mwingine wa ufahamu ambao ukiwa umekufa utapata ugumu sana, kupata taarifa ya kile kinachoingia ndani yako. Kwamfano kama chakula hakina chumvi, huwezi kukitambua kwa macho au mwonekano wake mzuri, bali kwa ulimi ndio utapata taarifa zote.

Vivyo hivyo na sisi rohoni, ndimi zetu zinapaswa ziwe hai. Ili tuweze pambanua aina ya chakula kinachoingia ndani yetu. Omba Bwana akupe;

**Uwezo wa kutema**

Yesu alipopewa siki, hakuinywa bali aliitema, chini kwasababu alijua si maji bali ni uchungu, ambayo ungemletea madhara.

*Mathayo 27:34 wakampa kunywa divai iliyochanganyika na nyongo; lakini yeye alipoionja hakutaka kunywa*

- ✓ Bwana akupe hisia ya kuyatambua mafundisho-hatarishi, na kuyakataa haraka iwezekanavyo moyoni mwako. Mafundisho ya manabii wa uongo na mashetani.

**Uwezo wa kuhisi utamu wa asali na kuila sana.**

Asali ni Neno la Mungu.

*Mthali 24:13 Mwanangu, ule asali, kwa maana ni njema, Na sega la asali lililo tamu ulionjapo. 14 Basi utaijua hekima kuwa tamu kwa nafsi yako; Ikiwa umekwisha kuiona; Ndipo itakapofuata thawabu; Wala tumaini lako halitabatilika.*

- ✓ Mwombe Bwana akuongezee uwezo wa kuhisi utamu wa Neno lake, ili upende kulisoma sana.

**Uwezo wa kuhisi ubora wa chakula.**

Chakula kikiwa cha moto au baridi, au kimechacha, ulimi utakusaidia kutambua hilo. Vivyo hivyo rohoni tunauwezo wa kutambua fundisho la wakati ufaao. Kwasababu yapo mafundisho yasiyo ya sasa. Bwana alisema waliozoea divai ya kale hawapendi divai mpya.

Kuenenda katika fundisho la sheria za kutoa kafara za mbuzi na kondoo wakati tunayo damu ya Yesu Kristo ni sawa na kula chakula kilichochacha. Kukosa kujua fundisho sahihi itakupelekea kusimamia mistari ambayo sio ya wakati husika, kwamfano Yesu alipojaribiwa na shetani na kuambiwa ajitupe chini kwasababu imeandikwa ataagiziwa malaika zake. Yesu alikataa fundisho lile kwasababu lilikuwa sio "fresh" kwa wakati ule, yeye akamweleza lile lililo "fresh" Kwamba usimjaribu Bwana Mungu wako.

- ✓ Omba Mungu akupe hisia hii ya rohoni, kutambua fundisho sahihi, au ufunuo sahihi wa wakati wako husika. Ulimi wako ujue kilicho cha moto na baridi, na wakati husika wa kuliwa.

## PUA (dk 75)

Pua hutambua harufu. Hata kama kitu hicho kimejificha kiasi gani, pua husaidia kutambua yote. Kwamfano ikiwa jirani yako amejifungia ndani anapika pilau. Utaweza kutambua anachokifanya kwa harufu tu.

Vivyo hivyo rohoni pua zetu ziwe nzima.

Vipo vingi vinatendeka lakini hatuvihisi, kwasababu tu hatuvioni.(Zaburi 115:4-8) Kwamfano unaweza Ukakutana na mtu asiye na nia nzuri. Usimtambue kwa haraka umwonapo kwa nje lakini harufu yake rohoni ikakutambulisha ni mtu wa namna gani. Hiyo ndio inaitwa AMANI YA ROHO.

Yapo mazingira sio rafiki kwetu sisi kukaa, au watu kushirikiana nao. Yapo mazingira kwa nje yataonekana ni mazuri lakini rohoni ni majalala, yanayotoa harufu mbaya.

- ✓ Mwombe sana Bwana aifungua pua yako ya rohoni, utambue uwepo wa kweli wa Roho Mtakatifu upo wapi. Na huo haupo pengine zaidi ya nyumbani mwake. Kwasababu huko ndiko harufu nzuri za manukato ambayo ni maombi na sala za watakatifu zinapotokea. Ndipo uvumba mzuri unapofukizwa.
- ✓ Akupe uwezo wa kuisikia harufu nzuri inayotoka walipo wawili au watatu kwa jina la Bwana. Ili uweze kukaa hapo

## NGOZI (dk 75)

Ngozi kazi yake ni kuhisi, haidha mguso, au hali ya mazingira, kama ni joto, au baridi, au raha au maumivu. Kama una hisia kwenye ngozi ukitembelewa na sisimizi kwenye shingo yako utajua, ijapokuwa hujamwona wala kumsikia.

Vivyo hivyo rohoni, ipo miguso mingi sana, na tukishindwa kuitambua tutapata hasara ya mambo mengi.

**Mguso wa ki-Mungu.**

Mungu huwa anawagusa watu, lakini hawahisi chochote. Wakati mwingi Mungu atakugusa uamke uombe, ukashuhudie habari njema, ufunge, usome Neno.

- ✓ Omba Bwana akupe wepesi wa kuitikia mguso wake, ili zisikupite Baraka zake

**Mguso wa mwanadamu mwenzako.**

Kuna wakati Yesu aliguswa na mwanamke mwenye shida ya kutokwa na damu akahisi rohoni ameguswa. Hivyo akamtafuta na kumsaidia huyo mwanamke zaidi.

*Luka 8:45  Yesu akasema, Ni nani aliyenigusa? Basi, watu wote walipokana, Petro alimwambia, Bwana mkubwa, makutano haya wanakuzunguka na kukusonga. 46  Yesu akasema, Mtu alinigusa, maana naona ya kuwa nguvu zimenitoka*

- ✓ Omba Bwana akupe kuhisi shida za wengine kwa wepesi uwasaidie, si tu mpaka pale utakapoambiwa.

**Mguso wa kipepo:**

Mapepo pia yanawagusa watu. Wanawawekea shinikizo ndani yao, kulaghai, au kutenda dhambi, au mambo yasiyompendeza Mungu. Yuda alikwenda kumbusu Yesu, lakini mguso ule haukuwa wa upendo bali wa kumsaliti. Lakini Bwana alitambua.

- ✓ Hivyo omba Bwana akupe kutambua miguso ya kipepo, ujiepusha nao.
- ✓ Usiwe mwepesi kuitikia miguso yote isiyo na uelekeo wa kuujenga ufalme wa Mungu.

Ukizingatia kuomba kwa bidii juu ya hivi vipengele kwa dakika hizo 75 , katika maombi yako basi rohoni utaingia katika kiwango kingine cha juu sana kwasababu umezingatia kuitibu roho yako kibiblia kama Bwana anavyotaka.

Bwana akubariki.

Toleo lingine litakuja wiki ijayo...

Na, Mwl Denis & Devis Julius
Nuru_ya_ Upendo
Website: www.wingulamashahidi.org
Email: info@wingulamashahidi.org
+255693036618/ +255789001312